# Mambo makuu kuhusu Viongozi Wema

**1. Wanafahamu kwamba uongozi ni ushawishi**

Uongozi ni vitu vingi, lakini asili yake ni ushawishi na hali ya kuweza kushawishi wengine. Kiini cha neno "ushawishi" haswa ni "kutiririka ndani" ya wengine. Kiongozi ni yule ambaye kwa kumaanisha "hutiririka ndani" ya wengine. Umaarufu wake kama kiongozi unategemea ushawishi wake. Kipimo cha uongozi wako unategemea idadi ya watu wanaoshawishika na uongozi wako kila siku, kila juma, kila mwaka, na maishani mwote.

**2. Wanafahamu kuwa uongozi ni kitu cha kuendelea**

Imesemekana kwamba viongozi hawaundwi bali huzaliwa. Hi ni ukweli nusu. Kuna wale wanaozaliwa na uwezo katika ungozi, lakini viongozi shupavu katika uliwengu wanafahamu kwamba uongozi huchukua muda kukua na inahitaji nithamu. Uongozi hukuzwa kila siku. Haikui kwa siku moja. Kwa hivyo uwe na bidii katika kuimarisha uongozi wako. Kuimarisha ujuzi wako katika uongozi kutakupa nafasi mwafaka wa ushawishi. Musa alianza kwa kumwambia Mungu, "Lakini Bwana, mimi ni kigugumizi, nitakwendaje kwa Farao na kuongea?" Baada ya kufundishwa na Mungu, na kuwa na imani, akaliongoza taifa! Alikuzwa ndani ya kazi. Unaweza kuzidisha ushawishi wako ikiwa utaweka akili yako na moyo wako kufanya hivyo.

**3. Wanafahamu kwamba ni wewe tu unayeweza kuweka kiwango katika ushawishi wako**

John Maxwell anaiita, "Kanuni ya kifuniko." Je, unataka kuwa na ushupavu wa namna gani kama kiongozi? Uamuzi wako utatoa mwelekeo na ushawishi wako na hatma yako kama kiongozi. Unaweza kuzidisha uongozi wako na ni wewe tu unayeweza kuamua kuhusu ushawishi wako. Inamaanisha kwamba uwezo wako unakutegemea. "Haya funga behewa kwa nyota, fungua macho na lahaula, umepata!" Watu wengi wenye uwezo mkubwa wanafanya mambo madogo madogo kwa sababu hawatambui uwezo walio nao. Usipunguze uwezo wako au yale ambayo Mungu anakusudia kupitia kwa maisha yako kwa kuwa mvivu au kwa kukosa kuitikia mwito zaidi.

**4. Wanafahamu kwamba mafuta yanayompa nguvu ni bidii ya moyo wake.**

Viongozi wana bidii katika mwelekeo wao. Wana moto ndani yao inayowasukuma kufanikiwa. Kiongozi "humalizwa" na maono yake au shauku yake, na ni sharti ashirikishe wengine. Uongozi hufundishwa na pia huigwa. Uwezo mwingi wa kiongozi uko katika hisia zake, kama vile tu uko katika akili na uwezo wake. Ni heri shujaa wa vita kuliko askari ambaye amefundishwa juu ya vita lakini hana moyo wa kupigana. Shauku hutangulia mipango kila wakati. Shauku na mipango huhitajika ili kuwe na ufanisi, lakini ni vigumu kumzuia kiongozi mwenye shauku.

**5. Wanafahamu kwamba viongozi ni Waelekevu na Wenye maono**

Nikiwa rubani wa ndege yangu, nilimuuliza mke wangu kama angelipenda kuendesha ndege. Alinijibu kwa kusema "ndiyo." Baada ya kushika duara ya kupindia ndege kwa dakika chache, aliniambia hivi: "Naweza kuendesha ndege lakini sijui ninakoelekea." Hii inatuambia kwamba mtu ye yote anaweza kuendesha ndege, lakini ni rubani tu anayeweza kuipa mwelekeo. Viongozi ni kama rubani wa ndege. Wana maono na mwelekeo. Kusema kiongozi ana mwelekeo na pia ni rubani ni kusema kwamba ni mtu "anayefikiria makuu." Kwa kawaida wao huwaachia watu wengine kushugulikia mambo madogo

madogo. Hiyo ndio sababu wasimamizi si viongozi. Wasimamizi hushughulikia tu mambo madogo madogo ya kila siku. Kiongozi anaona maono makuu kuliko “mkate wetu wa kila siku.” Anafikiri jinsi ya kutengeneza mikate ya kutosha kulisha ulimwengu!

**6. Wanafahamu kwamba viongozi wamejifunza mambo ya kutanguliza**

Yesu alituambia tutafute kwanza ufalme wa Mungu na haki yake (Mathayo 6:33). Hivi ndivyo ilivyo na viongozi shupavu. Wanafahamu vyema kuweka mambo ya maana mbele. Viongozi wana uwezo maalum wa kuzingatia mambo ya staha. Hawatoi jasho kwa mambo madogo madogo. Kuweka kipa umbele mambo ya staha, mda wako na uwezo wako ni kuwa na kipawa kizuri katika uongozi.

**7. Wanafahamu kwamba viongozi ni Watumishi, na si mabwana**

Katika kitabu kimoja kionachouza sana kiitwacho *Good to Great* tunajifunza kuwa mashirika yanayofahamika sana yana kiongozi ambaye ni mtumishi kwa watu wake. Hii ndiyo kanuni ya Yesu katika uongozi. Katika kitabu cha Yohana 13, tunaona kisa cha Yesu akiwa mtumishi kwa wanafunzi wake. Anawauliza hivi, “mnajua kwa nini nimefanya hivi?” . Kiongozi mwema ni yule ambaye hawezi kuuliza wafuasi wake kufanya chochote ambacho yeye mwenyewe hawezi kufanya. Wanajeshi wengi husimulia hadithi za jemedari waliowaongoza kwenda vitani. Akiwa amejiweka hatarini, yeye huongoza vitani. Kama vile Mel Gibson katika “*Brave Heart*” ambapo anamwonyesha William Wallace, bila woga, akiongoza watu wake katika pigano. Viongozi si mabwana, ila ni watumishi. Viongozi si nyapara au wasimamizi, bali ni wasaidizi katika unyenyekevu. Uongozi wao ni kutoka chini kwenda juu, wala si kutoka juu kwenda chini.

**8. Wanafahamu kwamba watu watamfuata mtu kabla kujitolea kufuata maono yake**

Mara nyingi viongozi chipukizi huwa na shauku sana kuhusu maono yao na hujaribu sana kushawishi watu wengine kukubali maono hayo na kuyafuata. John Maxwell anauita Kanuni ya “kununua.” Lakini watu wanapokosa kufuata au “kununua” maono yake, anashangaa ni kwa nini. Hi ni kwa sababu watu hufuata kiongozi kabla kukubali au kufuata maono yake.

Hebu fikiri jinsi Yesu alivyoongoza wafuasi wake. Alikaa nao kwa miaka mingi ili wamfahamu, wampende, na kisha wajitolee kumfuata. Hapo ndipo aliwapa maono yake. Viongozi shupavu wanafahamu kwamba watu humfuata MTU mwenye maono kabla kufuata maono yake. Kwa kuwa mnyenyekevu, mwenye maadili mema na mwelekeo, kiongozi ni kama sumaku anapovuta watu kwake. Kisha anawashurutisha kufuata maono yake.

9. **Wanafahamu kwamba kiongozi ni lazima avutie moyo wako kabla kuitisha msaada wako**

Viongozi shupavu wanafahamu kwamba siri ya kupata wafuasi ni kuaminika. Watu hawavutiwi sana na wazo la mtu, ila wanavutiwa na roho yake. Watu watakufuata wanapokuamini. Yesu alijua hivyo, na kabla kuwauliza wanafunzi wake wamfanyie kitu kama “kujitwika msalaba na kumfuata,” alihakikisha kwamba roho zao zilikuwa karibu naye. Kila wakati viongozi wakristo chipukizi huuliza watu misaada ya fedha na miradi bila kwanza kuwavutia, kwa uaminifu wake, wale wanaotafuta misaada kutoka kwao. Kwa mfano, mchungaji mwafrika anaweza kusikia kwamba huyu “mzungu” anawapenda waafrika na kwamba anasaidia makanisa na wachungaji kwa fedha. Kwa hivyo, bila hata kumfahamu huyu “mzungu,” anaanza kumtumia barua pepe kuhusu “maono yake” ya

kujenga makao ya watoto yatima. “Mzungu,” akisha pata taarifa ya mradi unaohitaji fedha kwa ajili ya watoto yatima, anafikiri hivi, “Ni nani huyu mwafrika ambaye simfahamu na ananiomba fedha? Simfahamu na hali anahitaji nimpe fedha za kutegemeza kazi yake.” Hebu nikuambie kwamba Yesu hangelifanya hivyo. Kiongozi mwema ni lazima aaminike kwanza kabla kuomba watu wengine kushikilia maono yake.

**10. Wanafahamu kwamba watu humfuata mtu wanayemheshimu**

Hii inaitwa “Kanuni ya Mzee” katika Afrika. Kwa lugha ya Kiswahili, “Mzee” ni mtu aliye na umri mkubwa na mwenye hekima. Yeye ni mkomavu na anaheshimika na wengi kwa hekima yake na yale ambayo amepitia katika maisha. Tamaduni za Kiafrika zina heshima kwa wazee. Tamaduni za kizungu huona wazee kama watu wasio na maana. Ingawa hiyo, kanuni katika uongozi ni kwamba watu hawatamfuata mtu wasiyemheshimu. Watu wanaweza kumwogopa kwa heshima na kuambatana naye, lakini kushika maono yake itakuwa vigumu ikiwa hawamwamini na kumheshimu. Kwa hivyo kiongozi mwema anaelewa kwamba itamgharimu muda na bidii kabla watu kumheshimu. Ujumbe wa maisha yake ni msingi katika uongozi wake. Kuongoza ni kwa tabia.

**11. Wanafahamu kwamba uongozi bora hutokana na uzalishaji**

Kiongozi shupavu anaweza kumwangalia mtu na kuona jeshi kubwa nyuma yake. Anajua kwamba akimtia moyo mtu huyo, na kumfunza kuongoza wengine, basi anaweza kujizalisha kwake kama mfuasi wake. Kiongozi anaweza kuona kwamba hesabu ya kuzidisha ni bora kuliko ya kuongeza. Itambidi kujizalisha kwa wengine ikiwa anahitaji kusambaza maono yake. Dawson Trotman, kiongozi shupavu wa wanaume wakristo, alikuwa na uzoefu wa kusema, “Utendaji hauwezi kuchukua nasafi ya kuzaa, na kuzaa kuchukua nafasi ya kuzalishana.” Mtume Paulo, ambaye pia ni kiongozi shupavu, alimwambia mfuasi wake chipukizi Timotheo kujizalisha kwa watu wengine waaminifu (2

Timotheo 2:2).

Usijiulize umekuwa ukifanya nini, bali jiulize, “watu wengine wanafanya nini kwa sababu ya yale nimekuwa nikifanya?” Viongozi wanazaliwa ili wazalishane. Yesu aliangalia wanafunzi wake kumi na wawili na kuona ulimwengu wote ndani yao! Aliwafunza na kuwapa Agano Kuu “kwenda na kufanya mataifa yote kuwa wafuasi...” Alielewa haja ya kiongozi kujizalisha.

**12. Wanaacha sifa njema**

Shauku ya kuzalisha maono yako kwa maisha ya wafuasi wako hutokana na haja ya kuacha sifa njema ukisha toweka. Kiongozi shupavu si yule anayeishi kwa “sasa,” bali anaishi kwa ajili ya kizazi kijacho. Katika Yohana 17, tunamwona Yesu akiwaombea wanafunzi wake, akisema, “*Siombi kwa ajili ya hawa tu, Baba, lakini nawaombea pia watakaoamini kwa ajili yao*.” Hebu ona kwamba alikuwa akiishi kwa kwa sifa njema kwa ajili ya vizazi vijavyo ambao wangeokolewa kutokana na uaminifu wa wafuasi wake. Viongozi shupavu wote huamini kwamba mwelekeo wao na maono yao yanafaa kupokezwa kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo viongozi hutoa muda wao bora kwa watu wao bora. Wanatazamia mabadiliko kwa siku za usoni. Wanaona maisha mema kutokana na wafuasi wao, walio na wafuasi wao, na wafuasi wao. Inawezekana kuwa unatengeneza sifa njema sasa au umeipuzilia mbali.